

K.C.S.E. MWONGOZO WA FASIHI – 2010

For More Free KCSE Revision Past Papers and Answers
Visit <http://www.joshuaarimi.com>

1. (a) i) kufungwa / kama mbuzi / mbwa
 - ii) kinyimwa uhuru
 - iii) alipofungwa pameharibika
 - iv) angependa kuhama lakini hawezি
 - v) kunamajani mengi mbele yake lakini hawezি kuyafikia – chakula
 - vi) analalamikia ufupi wa kamba
 - vii) analalamikia upungufu wa chakula / njaa / sahani imeenda mbali

ZOZOTE $4 \times 1 = 4$ (FUNGЕ)

- (b) i) amekwisha zoea hali yake
 - ii) hapendi kuonekana tofauti. Hataki kuukosa utu kwa sababu amefungwa katika kamba ya utu/ hana misimamo yak, analazimiswa na sheria, dini, itikadi n.k.
 - iii) madhara kama walivyofanya mbuzi na mbwa
 - iv) aweze kupata kisingizio au sababu ya kulalamika

YOYOTE = $1 \times 2 = 2$

- (a) Ni dhamiri katika nafsi yake ambayo ameshikilia abayo haionekani kwa macho ndiyo iliyomfunga / hajafungwa na yejote, amejifunga na nafsi yake.
- (b) i) tashbihi – kama mbuzi
 - kama mbwa

- ii) sitiari/ sitiari / jazada – sahani ya mbingu, kama isiyoonekana
 - mtu wa utu
- iii) tafsida / tauria – nimekwishapachafua
- iv) takriri / uradidi/ marudio /kusisitiz – kamba, kamba
- v) nidaa / siyahi - oh!
 - unuru!
- vi) tashihisi / uhuishi/ uhaishaji – dhamiri imenifunga
 - sahani kwenda mbali
 - mti wa utu
- vii) taswira – kamba fupi / mbuzi kuzunguka
 - mbwa kusukuma sahani mbali
- viii) tanakuzi – anataka kufunguliwa lakini tena hataki
- ix) kinaya – namshukuru aliyenifunga hapa
- x) nahau- msemo k.m. piga teke.

ZOZOTE $2 \times 2 = 4$ (FUNG)

- (c) mishata : mishororo ambayo maana yake inakamilika katika mishororo naofuata mf.
- i) Name kwa mbaya bahati, katika -----
 - ii) Uhuru kupigania, sahani ya mbingu-----
 - iii) Nimepiga teke na niigusapo kwa mdomo-----
 - iv) Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena-----
 - v) Name sasa sitaki ikatike maana-----
 - vi) Mbuzi wa kamaba alipofunguliwa, mashamba----

ZOZOTE $2 \times 2 = 4$

(d) i) nimefungwa kama mbwa na kwa bahati mbaya

- ii) katika kutaka kuondoa pale nimeipigiwa teke sahani ya mbingu
- iii) ambayo imeenda mbele na siwezi kuifiki
- iv) na pale nilipofungwa ni pachafu

AU

- i) mshairi analalamika kufungwa kwake kama mbwa
- ii) katika harakati zake za kupigania uhuru na kufanikiwa kuupata
- iii) alichotaka hata akizidisha bidii
- iv) mahali alipofungwa amepachafua na hawzi kupaondoka

UTENGANO

2. (a) i) haya ni maneno ya kazija

- ii) anamwambia Maksuudi
- iii) wamo nyumbani kwa Kazija

iv) maksuudi amekuja kumtembelea Kazija na kumfumania Muusa ambaye pia amekuja kumfuata Kazija, Maksuudi amempiga Muusa , Muusa ametoroka , Maksuudi amemwamia Kazija kuwa yeye Kazija si mwanamke, ndipo Kazija anamwambia Maksuudi maneno haya.

HOJA $4 \times 1 = 4$

(b) mtahini aonyeshe jinsi Maksuudi alivyowadhulumu wanawake

(i) Maimuna

- maksuudi amemzuia kuufahamu ulimwengu halisi/ amemtenganisha na ulimwengu / dunia ya nje
- alimnyima uhuru wa kuamua
- alimtawisha kwa muda mrfu
- alimlea kikatili
- anamnyima elimu – anamsomesha ndani
- kelele zake zilimzuia kufurahia mazingira shwari
- anamtesa kisaikolojia kwa kumtesa mamake- Tamima
- kupitia kwa Bi. Tamima, alisema nyumba yake aione paa.

(ii) Tamima

- Anamsaliti kimapenzi kwa kushirikiana kimapenzi na Kazija/ kuzini, na kazija
- Anamnyima uhuru wa kufurahia maisha ya ndoa, anamtusi akimwita paka.
- Alimnyima haki za binadamu kama huduma za daktari au mkunga – anamkataza mkunga kuingia nyumbani kwake.
- Anamuonyesha dhuluma, ukaili na hamaki – k.m. alimpiga na kujeruhi vibaya punde tu baada ya kujifungua.
- Kumjeruhi vibaya punde baada ya kujifungua
- Alimtaliki bila sababu na bila kuzingatia utaratibu
- Alimfukuza usiku

- Alinzuia kufanya kazi ya ujira
- Alimnyang'anya kitoto kichanga
- Alimtawisha / anamfungia nyumbani
- Anamwacha akiwa karibu kujifungua na kudhamiria kukaa kwa kazija kwa juma moja
- Kusababisha utengano kati ya Tamima na watoto wake
- Tamima kuishi kwa upweke.

(iii) Kazija

- Maksuudi na viongozi wengine wanamnyima Kazija na wanawake wengine nafasi katika elimu
- Anamtumia kama chombo cha starehe
- Anmdhulumu shoga yake Farashuu
- Anamdhalilisha kwa kumwambia wewe si mwanamke
- Mwanamke mwepesi wa kuliwa

(iv) mwana sururu

- Anamnyang'anya mali alioachiwa na babake
- Anamfanyia unafiki – anamwoa kwa kutaka mali yake na kumfanya kuingilia ukahaba
- Anamtaliki baada ya kumhini
- Alimpiga

- Alintawisha
- Alisababisha azae nje ya ndoa
- Alimsababisha kifo cha mapema

(v) Bi Farashuu

- maksuudi alimuoa mwanawe Mwanasururu
- Akamtesa na kumnyang'anya mali
- kusababisha kifo chake cha mapema
- kuishi kwa uchungu mwangi na kuwa chozi la muliwa ambalo lilitamatika baada ya kifo cha maksuudi
- uchungu wa kumwona kabi na mguu mmoja

(vii) Mkewajapu

- Maksuudi alipokuwa mkuu wa wilaya alitaka shilingi 200 kuweka sahihi apate kiwanja

(viii) Fikirini

- Ambaye alikuwa na woga na kushindwa kubanduka maksuudi alipokuwa akimpiga (Tamima) woga uliwajaa watumishi wengi kwa nyumba ya maksuudi na wakatoroka.

ZOZOTE $4 \times 1 = 4$ (FUNGE)

3. (a) i) uzungumzi nafsi hufokea ambapo muhusika anazungumza mwenyewe kwa mwenyewe au kimigomoy.

ii) kazija anaposubiri kuja kwa muusa na maksuudi nyumbani kwake.

Anajisemea,” huogopi mwanamke we!” “toka lini hata leo iwe ya pili” labda kazija “ uzungumzi huu unadhihirisha azma ya kazija na ujasiri / ukaidi wa kutekeleza mpango wa farashuu kuwafanya mtu na mwanawewe kufumaniana nyumbani kwake. Jambo hili linasababisha kutengana kwa maksuudi na mwanawewe musa na matukio mengine yote katika riwaya.

iii) maksuudi anapojisemea kwa kinywa kipana “ mabadiliko --- ! mwandishi ametimia mbinu hii kutubainisjia hali ambapo maksuudi anajutia matendo yake na yuko tayari kubdilika.

iv) Maksuudi anpojiuliza “lusu! Nani lusu? Lusu tamima au maksuudi?” lusu tamima au maksuudi mwenyewe?” anajiuliza maswali haya akiwa shambani mdhaifu wa afya baada ys kutoka kizuizini. Maksuudi

v) Maksuudi anaposema “la, la, la Nitakwenda kuwatafuta wanangu katika uhai wangu uliobaki” uzungumzi huu unaashiria mabadiliko katika maisha ya maksuudi na kusositiza azma ya kuwatafuta wanawewe. Jambo hili linaendeleza kadhia kufkia kilele / linaonyesha uwajibikaji wa maksuudi.

vi)Uk. 10. Kazija alisema kimoyomoyo kwa maksuudi alipotka kumjulia hali, “za huku mbaya”. –kuashiria kuwa siku hiyo amepanga kuwakutanisha na mussa hapo kwake.

- Maudhui ya uasherati

- vii) Uk. 18. Rashid juu ya yale ameyafanya siku hiyo “ leo nimekwenda marikiti kujenga taifa mimi na bwana”
- viii) Uk.23. “ radhi za wazazi ni fimbo kubwa ukizikosa” – kuonyesha maimuna hakutaka kuivunja amri ya babake lakini alilazimika. Utamaduni na heshima.
- ix)Uk.26. maimuna kuelezwewa/ kusifiwa juu ya mapenzi na biti kocho. Alishangaa ni mapenzi au mateso.
- x) Uk.45. tamima kusema kimoyomoyo, maimuna anataka kuwa kiparamotoukubwani. Ufawa haukumsaidia.
- xi)Uk.64.maimuna anapewa pesa na mama jeni. Alishangaa ni za nini na kusema ,”pesa? Za nini?”
- Kuonyesha ubichi wake katika mambo ya dunia baada ya kufungiwa miaka hii yote.
- xii) Uk.70. maksuudi alifanya mazoezi ya hotuba yake ambayo aliitoa siku ya kuomba kura. – majivuno na uongo.
- xiii) Uk. 71. Inspeksa fadhili alipokuwa akikagua vitu vipyta katika nyumba ya maksuudi. Ufisadi na ubadhilifu – utajiri wa upesiupesi
- xiv) Uk.78. – mzee japu alipolalamika juu ya maksuudi
- xv) Uk. 79. – zanga anapouliza kama kuna, bakari anajibu moyoni, “njia, kazi.....” – kuonyesha kuchoka kwa wananchi baada ya kudanganywa kwa miaka mingi.
- xvi) Uk.91. – “ni aside” – kueleza pombe iliyotumiwa na walevi wa bobea. – mali ya maimuna inaendelea kudorora
- xvii) Uk. 92. – maimuna kujilaumu eti maimuna anajiulizahivi, “kama si yeze aliyefunga safari ya meli”.

- xviii) Uk.94 “mpaka lini”. Akili ya maimuna ilisimanga. – kueleza maisha ya maimuna yalivyoendelea kudorora. Anaishi nakama.
- xix) Uk.102-3- maksuudi anazungumza na nafsi yake kuhusu maisha yake. “je, amefanya nini katika dunia hii? Ninamjulisha amefanya mengi lakini yota yalikuwa maovu. Na huu ni mwanzo tu wa kuporomoka; mwisho bado. “ – maovu kama kutesa familia yake, ujeuri, kuwatia watu uoga, kufanya watu wamchukie, kumtawisha maimuna na kusababisha kutoroka kwake, kusababisha mussa na tamima kutoweka. Ssa anaona umuhimu wa familia yake. Wangemuliwaza wakati kama huu. Anaamua kwenda kuwatafuta.
- xx) Uk. 106. Maksuudi sasa aliomba sala ya ukweli, “ mshibe mungu” – anaomba sasa sio kama zamanialippokuwa anaenda kwa kazija
- xxi) Uk.111.-selume analalamika juu ya shoka mme wake aliyemwacha jukumu la kulea watoto.
- xxii) Uk.135. binti sururu alisema kimoyomoyo, “uzuri wa” Akizungumzia urembo wa maimuna uliodorora.
- xxiii) Uk.137. “njoo njoo” Mwandishi kuelezea jinsi maisha ya dunia humzunguka mtu.
- xxiv) Uk.148. maimuna alijipa moyo, “ riziki za”. baada ya kuelezewa na shog yake mwanamkuu huko futoni kuwa maisha ya huko ni mfutomfuto.
- xxv) Uk,173. Baada ya maimuna kuolewa na kabi alifikiria juu ya suku yake ya harisi.
- xxvi) Uk.84. maimuna alijizungumzia kuhusu mahali pa kwenda baada ya kutoka kwa mama jeni lakini anasema si kwa bi. Tamima.

xxvii) Uk.169. farashuu kulilia mwanawe, “nani aliyemfisidi.”
Pale farashuu alipofika kwa kabi

xxviii) Uk.156 maimuna kupewa kolekole bila ya kuombwa
pesa na kabi

xxix) Maimuna kujiwazia kuwa debe bovu babake alippoenda
kumtafuta rumbaloia

ZOZOTE 5×

(b) Taswira

- i) Taswira ni picha inayojitokeza akilini mwa mtu anaposoma maandishi, anaposikiliza au kutazama jambo/ mtu Fulani – maana.
- ii) Maelezo kumhusu kazija yanayobainisha urembo wake wa kuvutia ambao unawavuta mussa na maksuudi na hatimaye kuwaponza na kuwatenganisha.
- iii) Maelezo kuhusu jumba la maksuudi la kifahari lilipmbwa kwa mapambo kutoka ulaya yaliyopatikana kutokana na shughuli za magendo. Maelezo haya yanadokeza maovu ya maksuudi na matendo yake hasa ya kuwatawisha mkewe na motto na kuwadhulumu wafanyakazi.
- iv) Taswira aliyokuwa nayo biti sururu ya maumbile ya maimuna – maelezo haya yanayoonyesha kuwa urembo wake maimuna ulikuwa umeanza kuchujuka na hivyo kutishia chanzo cha kipato chake. Wakati ulikuwa umefika wa yeze kutafakari hatua nydingine.
- v) Maelezo kuhusu mussa alipokuwa mvunguni nyumbani kwa kazija na vile alivyohisi akisikilizamazungumzo kati ya kazija na maksuudi
- vi) Taswira ya pale hotelini rumbalola. Yale maelezo hasa wakati bw. Maksuudi anatoke akijikokota kumsongelea maimuna kwa furaha ya uwezekano wa kumpata mwanawe lakini maimuna awakimbia kuzidisha utengano wao.
- vii) Taswira ya kipigo cha tamima kutoka kwa maksuudi kuonyesha ukatili wa maksuudi

- viii) Umbo / tambo la biti kocho kuonyesha ujasiri wake
- ix) Maelezo kuhusu – madongooromoka nyumba ya farashuu na vibanda vinavyoizungukwa kuonyesha utabaka.

ZOEOTE $5 \times 2 = 10$

KIFO KISIMANI

4. i) kabla ya kutokea jambo kuna ishara au dalili
- ii) Raia kususia mukutano wa bokono
- iii) Utawala kuanza kuwashuku raia kuwasingizia mambo kv. Mwelusi kusingiziwa kuchochea watu
- iv) washauri kutowajibbika huku wakisema uongo kwa mtemi bokono/ unafiki / sifa za uongo
- vi) Manung'uniko ya raia kuongezeka – k.m. dhidi ya kunyakuliwa kwa bonde la langi/ mama agoro / maji kisimani
- vii) Vitisho vyta watawala kwa wale wanaofikiriwa kuwa wanawachochera wananchi km. mwelusi
- viii) Wasiwasi wa bokono unampeleka kupata majinamizi/ndoto/askari II na wasiwasi wake
- ix) Viongozi kuharibu mazingira / unyakuzi wa kujifaidi na kuhisi wataondolewa utawalani
- x) Matusi, ukatili, mateso na dhuluma ya watawala kwa raia km. mwelusi gerezani/ mtuhumiwa.
- xi) Tendo la kuwaweka wananchi kizuizini km. mwelusi / mtuhumiwa
- xii) Propaganda/ kuvamiwa kwa balusi na batuitui eti ni nchi jirani
- xiii) Kuwajaza raia uoga km. mbute kulekezwa kwa batu / kuchoma nyumba / kuwapiganisha raia.

- xiv) Bokono kupuuza ushauri wa nyalwe anapoambiwa hapendwi na watu na washauri wake ni waongo
- xv) Kuwalazimisha raia kutangaza uzalendo wao km. mwelusi kuambiwa aseme ya kwamba "wapenda uongozi wa mtukufu mtemi bokono"
- xvi) Tenga tawala km. makabila kupiganishwa.
- xvii) Kutokuwepo uelewano baina ya askari na hali kadhalika viongozi km. kame na askari I
- xviii) Utawala kuwatenganisha kwa shughuli za upelelezi / batu kumpelekeza Tanya / bokono kutafuna mifupa ya askari.
- xxi) Watu kukaidi amri kama vile kuteka maji kisimani – mwelusi, andua , atega / bonde la ilangi / kisima cha mkomani
- xxii) Askari kupuuza amri kushambulia wandamanaji
- xxiii) Tanya kutowaambia aliko mwelusi – Tanya anakaidi
- xxiv) Raia kutolipwa kwa huduma watoazo – mbutwe kunyimwa haki
- xxv) Mauaji ya mwelusi ni tishio kwa uongozi
- xxvi) Maandamano yanayomn'oa bokono uongozini yanayoonyesha kuchoshwa
- xxvii) Njama ya kumtoa mwelusi gerezani – mkate wa wishwa/ pombe / umati
- xxviii) Ufisadi uwanja unanyakuliwa na mama agoro kulalamika.
- xxix) Ubaguzi / mapendeleo – motto wa kaloo kupewa kazi
 - xxx) Nyimbo za sifa za bokono kufifia / azena kuchelewa kufika kufanya kazi
 - xxxi) Ushawishi – gege na mwelusi
 - xxxii) Wasiwasi wa askari II

5.(a) i) nyalwe anazungumza

ii)Nna mumewe bokono

- iii) Wamo nyumbani / makao ya utawala
- iv) Anamdadisi kutambwa ni nini kinachomsumbu (ndoto) anamuelezzza maneno alixoyasema akiwa usingizini.

AU

- i) Haya ni maneno ya bokono akiwa usingizini
- ii) Nyalwe anakariri maneno haya kwa bokono
- iii) Wamo chumbani / makao ya utawala
- iv) Nyalwe amemuonya bokono kuhusu – uongozi mbaya – anamwambia bokonoana wasiwasi wa kuondolewa mamlakani, ndippo anatoa akizikwa akiwa hai.

$$4 \times 1 = 4$$

(b)

- i) Litifati – mbinu ya kuyanukuu maneno yaliyotamkwa au yaliyosemwa na mtu mwingine. Nyalwe anayanukuu maneno ya mtemi bokono
- ii) sitiari/jazanda- ulinganishi wa moja kwa moja. Shinda na matatizo / hofu ya mtemi. Kulinganishwa na kaburi
- iii) Kinaya – mbinu ya kusema kinyume au hali ya kuwa kinyume na ukweli / mtemi bokono ndiye anayeteswa si anayeteswa/ bokono anataka kuondolewa na hali yeye anatesa
- iv) Takriri – nitoeni nitoeni / udongo udongo
- v) Nidaa/ siyani – nitoeni!
- vi) Taswira – picha ya udongo kutoka kaburini au picha ya udongo kufukuliwa kaburini.

$$2 \times 2 = 4 \text{ (funge)}$$

- (a) Mtahiniwa aonyeshe kinyume cha matarajio / mambo yanayofanywa kinyume na hali inayotarajiwa.

- i) Utawala wa mtemi bokono unawatesa raia wan chi yake – kuwanyima raslimali – maji
- ii) Viongozi wanatumia nafasi zao kujiendeleza – ardhi ya watoto kuchezea inapewa askari mkuu
- iii) Askari polisi wanawatesa raia – mwelusi anapigwa na talui/ mweke.
- iv) Wanafungwa kunyimwa haki ya kutembelewa – mwelusi harihusiwi kuonekana na Tanya
- v) Raia wanawalazimisha kuhudhuria mikutano ya mtemi bokono
- vi) Raia hawana uhuru wa kumkosoa mtemi bokono / maadamano kusitishwa na polisi
- vii) Viongozi kuharibu mazingira / kukata miti
- viii) Viongozi wanawapiganisha raia / wanachoma nyumba zao ili wapigane – balusi/ batuitui
- ix) Mtemi bokono anajiona / anajielezakama kiongozi aliyeuleliwa na mungu
- x) Washauri kumkosoa bokono / kumpa sifa za uongo
- xi) Utawala kuwalinda wahalifu – askari wa pili na kikosi hawaulizwi chochote baada ya kumuua mtuhumiwa
- xii) Raia kutolipwa kwa huduma km. mbutwe
- xiii) Askari III na II kula chakula cha mfungwa
- xiv) Matumizi ya propaganda – batu / zigu kutaka kumuua mwelusi na kutangaza kuwa amekufa kwa ugonjwa wa moyo
- xv) Gege kumuua mwelusi / mtuhumiwa kuuliwa na askari waII
- xvi) Viongozi kuwatekeleza baadhi ya raia katika njaa na umaskini (matokeo ya kuharibu mazingira)

- xvii) Askari III kujaribu kumnyanyasa andua kimapenzi – anataka kumshika kifua
- xviii) Bokono kuwa anaruci nyuma badala ya kupevuka katika uongozi – nyalwe anaigiza bokono akirudi kutoka makamo – ujana – utotoo – kijusi tumboni mwa mama
- xix) Upendeleo/ ubaguzi mf motto wa kaloo kupewa kazi

$$\text{ZOZOTE } 6 \times 2 = 12(\text{FUNGE})$$

HADITHI FUPI

6.

(a)

- (i) Kauli hii inatolewa na mzee atanasi
- (ii) Alipokuwa njiani kutoka ofisini kwa mwalimu mkuu
- (iii) huku akiwaza, alikuwa amefika ofisini kuitika wito wa mwalimu mkuu
- (iv) katika mazungumzo mwalimu mkuu alimfahamisha atanasi kubadilika kwa tabia ya mwanawe nanda. Mwalimu alimuomba ajaribu kumchunguza mwanawe na kusema naye ili kufahamu tatizo lake maana walimu walikuwa wameshindwa. Jambo hili lilimfanya atanasi kuwaza mengi. ALAMA 4
- (b) Anayerejewa ni nanda mwanawe mzee atanasi – tatizo lilikuwa kubadilika kwa tabia kutokana na bamgi/ mihadarati/ dawa za kulevyta. ALAMA2

VITENDO VYA NANDA

- Kufika shulen iamechelewa
- Ulegevu/ kuzorota kiafya
- Kusinzia darasani
- Kukosa kuzingatia usafi, kutochana nywele
- Kudorora kwa matokeo kwenye mtihani

- Kuboboja darasani
- Kupata majinamizi
- Kubumburuka usingizini na kupiga mayowe
- Kuwa na macho mekundu
- Kuwa na wingi wa machachari/ makuruhu

$$4 \times 1 = 4$$

(c) mzee atanasi aliamini kuwa mwanawe amerogwa na jirani yake andanda – aliazimia pia kutafuta msaada wa waganga maarufu/ werevu. $2 \times 2 = 4$

(d) i) malezi yasiyofaa

- mzee atanasi babake
- kwa kutopata muda wa kukaa na kuchunguza mwanawe
- alimruhusu nanda kupata ajira

ii) tama – mzee makulu – mwenye duka – ndiye aliyempa nanda kazi ya kuchuuza bangi na kumshawishi avute ili alime mashamba vilivyo

iii) unafiki – alimficha mzee atanasi ukweli kuhusu hali ya mwanawe

iv) kukosa mapenzi ya mama – mama nanda – mchuuzi wa samaki – hakupata nafaasi au muda wa kukaa na kumshauri

v) hali ya umaskini iliyompelekea motto nanda kuwa mhitaji hadi akatafuta ajira

vi) ajira ya watoto – mzee makulu aliwaajiri nanda na wenzake

$$\text{ZOZOTE ZA KWANZA } 3 \times 2 = 6$$

7. KUFANANA

- i) Vyote ni vipersi vya semi katika fasihi simulizi
- ii) Zote ni kauli fupi fupi ambazo hutoa ujumbekwa kutumia taswira au picha kama kitendawili. Nyumba yangu haina mlango. Hapa tunaingiwa na taswira ya nyumba isiyo na mlango. Methali: motto akibebwa hutizama kisogo cha mamake. Inapotajwa, methali hii, tunaona picha ya motto alyebewba akitizama kisogo cha mamake,
- iii) Vyote huweza kutumia kugha ya mafumbo k.m. vitendawili. Methali; uvivu ni nyumba ya njaa.
- iv) Vyote huchota kutoka mazingira au jamii hisika. Hutumia kutekeleza majukumuyanayofanana, mathalani vyote hutumika kuelimisha wanajamii, kuburudisha na pia kuendeleza utamanduni wa jamii.
- v) Vyote hukuza lugha.
- vi) Vyote hutumia tamadhalani ya usemi mf. Istiari, jazanda nk. Km. mgeni ni kuku mweupe. Mle nyumba ya udongo sihimili kishindo – methali. Kitendawili – samaki wangu anaelea kimgongo mgongo – mende.

Tashihishi;

Kitendawili – amchukuapo hamrudishi – kaburi.

Methali – chui naye ana mkwe au udungu wa nazi hukutania chunguni.

Takriri;

Kitendawili – huku fungu huku fungu katika bahari – nazi

Methali – chururu si ndo! Ndo!

Tanakali za sauti;

Kitendawili – huku ng'o na kule ng'o – giza

Methali – ndo ndo ndo hujaza ndo

Kinaya;

Methali – hidi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wako/ penye miti hapana wajenzi

Kitendawili – likitoka halirudi – neno au ana meno lakini haumi – kitambi
Takuzi;

Methali – aliye juu mngoje chini.

- vii) Vyote huelimisha jamii
- viii) Vyote huburudisha jamii
- ix) Vyote huchemsha bongo
- x) Vyote huleta umoja
- xi) Vyote huonya.
- xii) Vyote hukosoa
- xiii) Vyote huhifadhi utamanduni wa jamii
- xiv) Vyote hujasirisha
- xv) Vyote huhimiza
- xvi) Vyote hufariji/ huliwaza jamii
- xvii) Vyote husaidia kukuza vipawa vya ulumbi
- xviii) Vyote hupokezwa kutoka kizazi hadi kingine
- xix) Vyote mali ya jamii, haina humiliki
- xx) Vyote vina pande mbili.